



**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 29 Mei, 2023**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi  
na Dua zitasomwa.

**I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka 2023/2024.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka 2023/2024.

**II. MASWALI:**

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

218. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahiki pongezi kwa kazi nzuri inayoifanya ya kuimarisha makaazi ya wananchi kuwa bora kwa kuchukua hatua za kuyafanyia ukarabati majengo ya nyumba za Michenzani. Hata hivyo kasi ya ukarabati wa majengo ya nyumba hizo imekuwa ndogo sana na inachukua

muda mrefu kumalizika.

- (a) Je, kuna tatizo gani linalosababisha kasi ya ukarabati wa majengo ya nyumba za Michenzani kuwa ndogo.
- (b) Je, mpango gani Serikali imeupanga katika kuharakisha ukarabati wa nyumba hizo ili kuongeza mandhari ya kuvutia ya jiji la Zanzibar.
- (c) Je, mpango wa kuyakarabati majengo yote ya nyumba za Michenzani unategemewa kukamilika wakati gani.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

196. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Pamoja na jitihada na azma ya Serikali ya kutaka kuwapatia vijana ajira za staha, bado idadi ya wanaohitimu na fursa za kazi zilizopo hazitoshelezi. Hata hivyo, pamoja na wito wa Serikali wa kuwataka vijana wajajiri, bado mazingira ya sasa sio wezeshi.

- (a) Je, ni upi mpango wa Serikali katika kuboresha vituo vya mafunzo ya amali na elimu mbadala ili kuwawezesha vijana kujiajiri wenyewe katika sekta mbali mbali.
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapa vijana uwezo wa kubuni miradi ya maendeleo ili waweze kujiajiri.
- (c) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kubuni njia bora za kuinua sekta ya sanaa na michezo kama ajira.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

55. MHESHIMIWA SAID SALEH SALIM (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Wananchi wa vijiji vya Bule, Chimba, Chanjaani na Utaani wanaipongeza sana Serikali kwa kuwafikishia huduma ya umeme. Hata hivyo, bado wanalo tatizo la kupatikana umeme mdogo linalosababishwa na kuzidiwa kwa transfoma iliopo Chimba Gombani.

- (a) Je, kwa muda gani sasa Wizara yako inalifahamu tatizo hilo.
- (b) Kwa kuwa tatizo hilo ni la muda mrefu sana Je, Wizara yako ina mpango upi wa haraka wa kulishughulikia tatizo hilo.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

242. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) -  
Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Hivi karibuni katika mitandao ya kijamii kumekuwa na taarifa ya kuonekana mamba katika mwambao wa bahari ya Kiwengwa iliyopo Kaskazini Unguja. Kwa kuwa mamba sio rafiki na harakati za kibinaadamu, na kwa kuwa shughuli za utalii kwa kiasi kikubwa hutegemea fukwe ambazo sasa zinatia hofu kutokana na kuonekana mamba huyo.

- (a) Je, ni ipi kauli ya Serikali juu ya uhakika wa kuonekana kwa mamba huyo.
- (b) Je, mamba huyo aliyeonekana alichukuliwa hatua gani na kwa nini ameonekana huko.
- (c) Ni hatua zipi Serikali imezichukua kuwapa taarifa za matumaini wananchi wa nchi hii, hususani wakaazi wa maeneo ya karibu ya fukwe juu ya hatari nyengine ya kupatikana mamba katika maeneo yao.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

186. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) -  
Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kwa mujibu wa bajeti na vipaombelevya Serikali kwenye utalii, Je, ni maeneo gani hasa Serikali imewekeza zaidi katika kuongeza watalii nchini.

**III. HOJA ZA SERIKALI:**

**Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka 2023/2024.

Zanzibar,  
29 Mei, 2023.

  
(Raya Issa Msellem)  
**KATIBU WA BARAZA**